Dart Jarida

DART
DAR RAPID TRANSIT AGENCY

Usafiri wa Umma Nadhifu

BRT Habari | Toleo la **6** | Julai - Septemba, **2026**







Rais Dkt. Samia awataka wananchi kulinda Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka

UK. 3

Fahamu Miundombinu ya Mradi wa DART Awamu ya Pili

UK. 4

TAHARIRI



BODI YA WAHARIRI

MWENYEKITI
Bw. Said Tunda

WAJUMBE
Shaban Kajiru
Elias Malima
Martha Komba
Sister Annestazia Msami
Kennorton Luhindi
Emmanuel Kapanga
Hellen Msovella
Salum Mtonga

MPIGA PICHA
Betram Moody

MSANIFU
Imani Charles

Jarida linaandaliwa na

Kitengo cha Mawasiliano
Serikalini Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Ubungo Maji, Barabara ya Morogoro
S.L.P 724, 16103 Dar es Salaam

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) ni Wakala wa Serikali ulioanzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 120 la tarehe 25 Mei 2007 chini ya Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya mwaka 1997 pamoja na marekebisho yake. Kwa sasa, Wakala huu uko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI).

DART ilianzishwa kwa lengo la kupanga, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mfumo wa kisasa wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) jijini Dar es Salaam ambao unatekelezwa katika Awamu Sita.

Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka umeendelea kuwa tegemeo kubwa la usafiri wa umma katika Jiji la Dar es Salaam sio tu kuhakikisha watumiaji wanafika shughuli zao za kila siku na kwenye shughuli zao za kila siku kwa wakati, lakini pia ni kichocheo kikubwa cha ukuaji wa Uchumi wa Taifa na kwa mwananchi mmoja mmoja.

Kutokana na umuhimu wa usafiri wa Mwendokasi, DART kwa kushirikiana na watoa huduma wake ambao ni Kampuni za UDART na MOFAT wameendelea kuboresha huduma kwa kuweka mabasi mapya na ya kisasa ambayo yanaendelea kutatua kero ya usafiri, kuondoa msongamano wa magari jijini sambamba na uhifadhi wa mazingira kwani mabasi haya kwa sasa yanatumia nishati safi ya Gesi asilia (CNG).

Katika mfululizo wa matoleo mbalimbali ya jarida hili, wananchi na watumiaji wa huduma ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka watapata taarifa mbalimbali hususani namna ya kutumia Mabasi ya BRT, elimu kuhusu matumizi sahihi ya miundombinu,Kadi Janja, Program tumizi ya Mwendokasi (Mwendokasi App) pamoja na kanuni, sheria na taratibu zote zinazosimamia mradi huu wa kimkakati wa Serikali.

Aidha, katika mfululizo wa majarida yetu wanachi watapata kufahamu shughuli zote za usimamizi wa watoa huduma katika mradi.

DART kama mdau mkubwa wa usafiri mijini anatekeleza kwa vitendo miongozo ya kitaifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na miongozo ya kisekta katika usafiri wa umma hivyo basi ni jukumu la Wakala kuhakikisha usafiri wa umma mijini unakuwa nadhifu na wa viwango vya kimataifa.

Katika toleo letu hili la Mwezi Julai hadi Septemba utapata kufahamu kwa undani maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa uzinduzi wa Awamu ya pili ya Mradi wa DART kuelekea Mbagala, maoni mbalimbali ya wananchi walipotembelea katika banda la DART na Ofisi ya Waziri Mkuu katika Maonesho ya Sabasaba na Nanenane, pamoja na kupata Elimu juu ya mradi wa BRT kwa ujumla.

Kwa kuwa jarida hili pia ni njia mojawapo ya kupata mrejesho kutoka kwa wasomaji na wateja wetu wa Mabasi Yaendayo Haraka, kukiwa na malalamiko, maswali, maoni au kuhitaji ufafanuzi zaidi kuhusu mradi wa DART tafadhali wasiliana nasi kwa namba yetu ya huduma kwa mteja ambayo ni bure **0800110147.**

Pia katika kurasa zetu za mitandao ya kijamii ya Facebook, Instagram, X na Linkedin kwa anuani za *@DARTMwendokasi* na kupitia barua pepe ya *mteja@dart.go.tz.*

Nawatakieni nyote usomaji mwema wa jarida hili.

"DART Usafiri wa Umma Nadhifu"

Said H. Tunda
Mtendaji Mkuu Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka

Rais Dkt. Samia awataka wananchi kulinda Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan amewataka wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na viunga vyake kuilinda miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka kwani inajengwa kwa thamani kubwa.

Akizungumza tarehe 7 Agosti, 2026 wakati wa hafla ya ufunguzi na uzinduzi wa Mradi wa DART Awamu ya Pili kuelekea Mbagala katika eneo la Kwa Azizi Ali Temeke Jijini Dar es Salaam, Mhe. Rais alisema kila mwananchi ni lazima awe mlinzi namba moja wa miundombinu ambayo Serikali inaijenga kwa fedha nyingi za Wafadhili na za Walipa kodi ambayo lengo lake ni kuwapunguzia adha ya usafiri wakazi wa Jiji la Dar es Salaam.

“Ndugu zangu Watanzania wajibu wetu ni kuilinda Miundombinu hii tunayoijenga. Tuilinde na matumizi yasiyofaa, hujuma na uharibifu wa makusudi” alisema Mheshimiwa Rais

Wakati wa uzinduzi huo, Mhe. Rais alisafiri kwa Basi la Mwendokasi kutoka Kituo cha Water Front hadi kwenye eneo la uzinduzi wa Mradi kwa Azizi Ali, sambamba na kutumia Kadi Janja ya Mwendokasi.

Aidha Mhe.Rais aliuelekeza Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) kuharakisha mchakato wa upatikanaji wa mtoa huduma ya mabasi katika Awamu ya Tatu ya Mradi unaoelekea Gongo la Mboto ili wananchi wa uelekeo huo nao waweze kufaidika na huduma za Mwendokasi.



“Nichukue fursa hii kuwaelekeza DART kuhakikisha wanatafuta mtoa huduma ya mabasi kule kwenye Awamu ya Tatu Gongo la Mboto kwa kuzingatia mahitaji halisi ya wananchi wa maeneo hayo” Alisema Dkt.Samia.

Mhe. Rais pia aliutaka Wakala DART kuhakikisha unatatua changamoto ya usafiri kwenye maeneo yenye uhitaji mkubwa wa mabasi hususani nyakati ambazo kuna uhitaji mkubwa ili kuondoa kero ya msongamano wa abiria kwenye maeneo hayo.

“Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) muongeze mabasi katika maeneo kulingana na mahitaji halisi ya abiria, kuna maeneo bado ukipita unakuta kuna makundi mengi ya watu wanasubiri lakini kuna mabasi yapo hayana kazi. Nataka muongeze mabasi maeneo ambayo abiria ni wengi na wanasubiri ili kupunguza muda wa kusafiri.”

> **“Nichukue fursa hii kuwaelekeza DART kuhakikisha wanatafuta mtoa hduma ya Mabasi kule wenye awamu ya Tatu Gongolamboto kwa kuzingatia mahitaji halisi ya wananchi wa maeneo hayo”**
> **Alisema Dkt. Samia.**

FAHAMU MIUNDOMBINU YA MRADI WA DART AWAMU YA PILI

Barabara	Eneo	Urefu (km)
Kilwa	Kutoka Kituo Kikuu cha Mbagala hadi Kituo Kikuu cha Gerezani	12.9
Gerezani	Kutoka Mtaa wa Bandari hadi Mtaa wa Sokoni awamu ya 1	1.4
Chang'ombe / Kawawa	Kutoka 'Mgulani JKT hadi Magomeni	6.3
	Jumla	**20.3**



Ufadhili

Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB)

Dola za Kimarekani Milioni **141.71**

Sawa na Shilingi za Kitanzania **Bilioni 217 na milioni 481**

1 Fungu la Kwanza — Kazi za

i. Barabara za mabasi

ii. Barabara za magari ya kawaida

iii. Njia za waendao kwa miguu

iv. **Madaraja ya vivuko 1**
Mbagala rangi tatu

v. Vituo vya mabasi 26

vi. **Barabara za juu 2**
eneo la Uhasibu na VETA

Hadi sasa ujenzi umekamilika asilimia 100



2 Fungu la Pili — Kazi za majengo

i. **Ujenzi karakana 1**
Mbagala

ii. **Ujenzi wa vituo vikuu vya mabasi 2**
Gerezani na Mbagala Rangi Tatu

iii. **Ujenzi wa vituo mlishi 4**
Zakhem, Mtoni kwa Azizi Ali, Duce na Misheni





Ujenzi ulianza rasmi mnamo tarehe 1 MACHI, 2019

> **Nimeona vijana wengi wanafanya kazi kwenye Vituo wakati napita hii ndio maana halisi ya maendeleo kwani uwepo wa mradi huu umewawezesha kupata ajira na hatimaye kujipatia kipato"**
>
> **Alisema Dkt.Samia.**



Rais Samia akoshwa na Mradi wa Mwendokasi katika kukuza Ajira.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan amepongeza uwepo wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili kwa namna ulivyoweza kuongeza fursa za ajira kwa vijana ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe.Rais alisema kuanza kwa utekelezaji wa mradi huo sio tu kumewapunguzia adha ya usafiri wakazi wa Mbagala na maeneo ya jirani bali kumeongeza ajira kwa vijana.

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili mapema mwezi Agosti mwaka huu, Rais Samia alionesha kufurahishwa na idadi kubwa ya vijana walioajiriwa kwenye mradi huu.

"Nimeona vijana wengi wanafanya kazi kwenye Vituo wakati napita hii ndio maana halisi ya maendeleo kwani uwepo wa mradi huu umewawezesha kupata ajira na hatimaye kujipatia kipato" Alisema Dkt. Samia.

Kwa upande wake Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Dkt. Sid Ould Tah alimhakikishia Rais Samia kuwa Benki ya AfDB itaendelea kufadhili miradi mikubwa ya maendeleo ambayo inaleta suluhisho la changamoto zinazowakabili wananchi kama ilivyo kwa mradi huo Awamu ya Pili.

Baadhi ya fursa za ajira zinazopatikana katika mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka ni pamoja na ulinzi, ufanyaji usafi, ukusanyaji nauli kupitia mifumo ya kidigitali, usaidizi wa abiria pamoja na udereva.



Bodi mpya ya ushauri yazinduliwa kukuza usafiri wa umma Dar es Salaam



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI Mhe. Prof. Riziki Shemdoe

Katika kuendelea kuleta mageuzi makubwa kwenye sekta ya usafiri wa umma na kuharakisha maendeleo ya Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mhe. Prof. Riziki Shemdoe, amezindua rasmi Bodi ya Ushauri ya Wizara kwa Wakala wa Mabasi ya Yaendayo Haraka (DART).

Uzinduzi huu wa kihistoria ulifanyika tarehe 31 Julai 2026, unaleta safu mpya ya viongozi na wataalamu bobezi wenye jukumu la kusimamia, kushauri, na kuleta matokeo chanya yatakayoboresha safari za mamilioni ya wakazi wa Dar es Salaam wanaotumia mfumo huu kila siku.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Prof. Shemdoe aliwataka wajumbe wapya kuacha maneno na badala yake wajikite katika utendaji kazi wenye tija utakaoupa nguvu mradi huu wa kimkakati.

"Baada ya leo uteuzi umeisha. Kilichobaki ni matokeo ya kazi yenu. Baada ya miaka mitatu tujipime tumeongeza nini kwa DART," alisisitiza Prof. Shemdoe.

Waziri Shemdoe aliiagiza bodi hiyo mpya kutekeleza vipaumbele kadhaa vya kimkakati, ikiwa ni pamoja na Kutathmini mfumo bora wa uendeshaji ili kutoa huduma iliyo bora zaidi kwa abiria pamoja na Kuongeza vyanzo vya mapato ili kuimarisha uwezo wa kifedha wa Wakala.

Vilevile Waziri Shemdoe aliongeza kuwa Bodi iandae DART kuwa mamlaka ya kitaifa ili kusimamia usafiri wa kasi nchini kote pamoja na kupendekeza maboresho ya sera na sheria pamoja.

Bodi hii mpya inaundwa na wajumbe wenye uwezo mkubwa na uzoefu wa kutosha katika nyanja mbalimbali za kitaalamu. Viongozi na wajumbe

> **“**
>
> **Tutafanya kazi bega kwa bega na Waziri na Menejimenti ya DART. Tutatoa ushauri wa kitaalamu na kupitia Mpango Mkakati ili kuleta tija inayokusudiwa," aliahidi Bw. Kafulila.**

walioteuliwa ni Bw. David Zacharia Kafulila, Dkt. Nicolaus Herman Shombe, Bw. Awadhi Juma Saidi Suluo, Dkt. Samuel Mwita Nyantahe, Dkt. Hassan Bashiru Shelukindo na CPA. Mohammed Mwandege Salami.

Akizungumza kwa niaba ya wajumbe, Mwenyekiti wa Bodi, Bw. David Kafulila, aliishukuru Serikali kwa imani kubwa iliyoonyesha kwao na kueleza kuwa DART ni taasisi ya kimkakati kwa uchumi na maisha ya wananchi.

"Tutafanya kazi bega kwa bega na Waziri na Menejimenti ya DART. Tutatoa ushauri wa kitaalamu na kupitia Mpango Mkakati ili kuleta tija inayokusudiwa," aliahidi Bw. Kafulila.

Kwa upande wake, Dkt. Nicolaus Herman Shombe, akizungumza kwa niaba ya wajumbe wenzake, alisisitiza dhamira yao ya dhati ya kushirikiana na wadau wote kuhakikisha huduma ya usafiri wa umma inazidi kuboreshwa na kuleta unafuu mkubwa kwa abiria.

Kwa upande wake Mtendaji Mkuu wa DART, Bw. Said Tunda, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji na mafanikio ya Wakala huo, aliahidi kuwa Menejimenti iko tayari

DART yang'arisha maonesho ya SabaSaba 2026



Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) ulipamba maonesho ya 50 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (SabaSaba), kupitia ushiriki thabiti na utoaji wa huduma ya usafiri wa haraka, salama na wa kuaminika kuelekea Viwanja vya Maonesho vya Mwalimu Julius Nyerere.

Maonesho hayo, yaliyozinduliwa rasmi Julai 3, 2026, na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, yalianza tarehe 28 Juni 2026 kabla ya kuhitimishwa rasmi tarehe 13 Julai 2026 na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

Katika maonesho hayo, DART ilishiriki kwa mtindo wa kipekee tofauti na miaka ya nyuma kwa kuandaa banda jumuishi lililomkutanisha pamoja na watoa huduma wake wa mabasi, Kampuni ya UDART na MOFAT.

Aidha, ushiriki wa DART haukuishia hapo; Wakala ulishiriki pia kupitia banda jumuishi la Ofisi ya Waziri Mkuu, chini ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), yote ikiwa na lengo la kusikiliza kero na maoni ya wananchi, kutoa elimu, na kuonesha mikakati ya kuboresha huduma za usafiri wa umma.

Akihojiwa na vituo vya televisheni vya TBC 1 na UTV wakati wa maonesho hayo, Mtendaji Mkuu wa DART, Bw. Said Tunda, aliwahimiza wananchi kutembelea banda la Wakala huo ili kufahamu kwa undani shughuli za usafiri wa umma wa kisasa, unaotambulika kama uti wa mgongo wa jiji la Dar es Salaam.

"DART tumekuja kuelezea kwa ujumla huduma zetu kwani changamoto tunayoiona ni kwamba walio wengi hawafahamu DART ni nini, UDART ni nini, Mofat ni nini, hata jinsi ya utoaji wa huduma," alisema Bw. Tunda. "Hivyo tunategemea maswali kutoka kwao ili waweze kujua."

Mwitikio wa wakazi wa Dar es Salaam ulikuwa mkubwa, ukichochewa na kurahisishwa kwa usafiri wa moja kwa moja kuelekea viwanjani hapo kutoka maeneo mbalimbali kama Mbagala, Ilala Boma, Kimara, Kivukoni, na Gerezani.

Kuthibitisha mwitikio huo chanya, katika kipindi chote cha maonesho kuanzia tarehe 28 Juni hadi 13 Julai 2026, jumla ya abiria 52,617 walitumia huduma ya usafiri wa mabasi yaendayo haraka kupitia Kituo cha SabaSaba. Katika idadi hiyo, abiria 46,155 walikuwa ni watu wazima huku abiria 6,462 wakiwa ni wanafunzi.

Wananchi waliotembelea banda hilo walieleza kufurahishwa kwao na huduma zinazotolewa. Bi. Esther Lema, mkazi wa Mbagala, alieleza jinsi usafiri huo ulivyoboresha maisha yake ya kila siku:

"Sasa naweza kutoka nyumbani na ndani ya dakika chache nikafika kazini, tofauti na awali ambapo tulilazimika kuzunguka na daladala au kugombea usafiri hadi kupandia madirishani," alisema Bi. Esther. "Hata ujio wangu hapa kwenye maonesho umekuwa mwepesi kwasababu ya Mwendokasi. Tunaishukuru Serikali kweli kweli."

Naye Bw. Idrisa Suleiman, mkazi wa Gongo la Mboto, aliipongeza DART kwa huduma nzuri na kutoa wito kwa wakala huo kupanua wigo hadi maeneo yenye changamoto kubwa za usafiri. "Huduma yenu ni nzuri sana. Tunaomba ifike na maeneo mengine kama Gongo la Mboto kwani tunapata shida kubwa ya usafiri, hasa nyakati za asubuhi na jioni," alisisitiza Bw. Idrisa.

Wageni 1,500 walisaini Kitabu cha Wageni kwenye banda la DART, huku wengi wao wakivutiwa na hatua kubwa za kidijitali zilizofikiwa na wakala huo.

Abiria sasa wanaweza kujihudumia wenyewe kupitia app ya simu ya kujikatia tiketi ya (Mwendokasi App) na kujijazia salio kwenye App hiyo au Kadi za Mwendokasi.

Katika kipindi hicho cha maonesho, elimu iliyotolewa na Maafisa wa DART kuhusu App ya Mwendokasi iliwafikia wananchi wengi, ambapo abiria 6,093 walifanikiwa kupakua programu hiyo kwenye simu zao za mkononi.

Hatua hizi zote zinajengwa juu ya msingi imara uliowekwa tangu Oktoba 12, 2025, ambapo huduma ya mabasi yaendayo haraka kwenye Mradi wa DART Awamu ya Pili ilianza kutolewa rasmi katika Barabara ya Kilwa, na hivyo kuendelea kuchochea ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja na jiji la Dar es Salaam kwa ujumla.

DART yakutanisha Wadau Kutatua changamoto za usafiri wa Mwendokasi



Wakati Jiji la Dar es Salaam likizidi kusonga mbele katika kuboresha usafiri wa umma, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) umewakutanisha wadau wake wakuu ili kujadili na kuweka mikakati ya kudumu ya kutatua changamoto mbalimbali zinazokwamisha au kuathiri ufanisi wa mradi huo muhimu kwa wakazi wa jiji.

Kikao hicho kilileta pamoja taasisi na wadau muhimu, wakiwemo Jeshi la Polisi (Kikosi cha Usalama Barabarani), LATRA, TANROADS, Kampuni ya UDART, Kampuni ya Mofat, Kampuni ya Ulinzi ya CT, Kampuni ya Ulinzi ya URA, pamoja na wawakilishi kutoka Manispaa za Ilala, Kinondoni, Ubungo, na Temeke. Akifungua kikao hicho, Mtendaji Mkuu wa DART, Bw. Said Tunda, alisisitiza umuhimu wa wadau hao kushirikiana kwa karibu ili kuweka uelewa wa pamoja kuhusu wajibu wa kila taasisi na kukubaliana hatua mahsusi zitakazosaidia kuimarisha ufanisi na usalama.
“Nawakaribisha katika kikao kazi hiki ambacho tutajadili na kuweka uelewa wa pamoja kuhusu wajibu wa kila taasisi, na kukubaliana hatua mahsusi zitakazosaidia kuboresha ufanisi na usalama katika uendeshaji wa Mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka,” alisema Bw. Tunda.

Bw. Tunda aliongeza kuwa Dar es Salaam ni kitovu cha biashara nchini Tanzania, hivyo usafiri wa mabasi yaendayo haraka ni tegemeo kubwa katika shughuli za kiuchumi, na endapo utatetereka utaleta athari kwa nchi nzima.

“Ukizungumzia Tanzania, unaizungumzia Dar es Salaam; hivyo isipotengemaa, viongozi wetu hawalali,” alisisitiza.
Aidha, Mtendaji Mkuu huyo aliwakumbusha wadau hao kuwa wao si washindani bali ni washirika. Alisema kuwa kwa kushirikiana, watapunguza vyombo vya moto vinavyovamia njia za BRT, jambo litakalosaidia kuepusha ajali na kuzuia mabasi kuchelewa kwenye ratiba hatua itakayopunguza malalamiko ya abiria ya kusubiri muda mrefu vituoni.
“Tunaamini dharura zipo, na taarifa ni muhimu kwa wasimamizi. Sasa ukijiamulia kupita tu kwa kisingizio cha udharura, je, kule ambako hakuna BRT wanapitaje?” alihoji.
Bw. Tunda aliwasihi wadau wanaotoa huduma kusikiliza kwa makini kile kinachozungumzwa na abiria wa mabasi yaendayo haraka na kuchukua maoni yanayowezekana ili kuyafanyia kazi.
“Mteja aliyekasirika ndiye mzuri

> **“**
>
> **Mteja aliyekasirika ndiye mzuri atakayekusaidia kuboresha huduma zako. Tusikilize zaidi kuliko kuongea,” aliongeza.**

abiria ya kusubiri muda mrefu vituoni.
“Tunaamini dharura zipo, na taarifa ni muhimu kwa wasimamizi. Sasa ukijiamulia kupita tu kwa kisingizio cha udharura, je, kule ambako hakuna BRT wanapitaje?” alihoji.
Bw. Tunda aliwasihi wadau wanaotoa huduma kusikiliza kwa makini kile kinachozungumzwa na abiria wa mabasi yaendayo haraka na kuchukua maoni yanayowezekana ili kuyafanyia kazi.

Akiainisha changamoto zinazoathiri utoaji wa huduma, Meneja wa Uendeshaji wa DART, Dkt. Katondo Nambiza Mzee, alisema kuwa ni pamoja na uvamizi na matumizi yasiyoruhusiwa ya njia za BRT,Mabasi ya BRT kutopata kipaumbele katika baadhi ya makutano, masuala yanayohusu usalama wa waenda kwa miguu, na utaratibu na mpangilio wa daladala katika maeneo yanayohudumiwa na mfumo wa BRTKikao hicho kimeacha matumaini makubwa kwa wananchi wa Dar es Salaam, kwani kimezalisha maazimio ya pamoja ya kudhibiti uvunjifu wa sheria na kuimarisha usalama barabarani. Hatua hii inadhihirisha wazi kuwa DART haipo tayari kuona kasi ya maendeleo ya usafiri wa umma ikizuiliwa, bali

DART yaimarisha usafi na kukabili mafuriko kwa ununuzi wa Gari la Kisasa la Maji Taka



Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) umezidi kujiimarisha katika kuboresha huduma za usafiri kwa kununua gari jipya na la kisasa la kunyonya maji taka, litakalotumika kutoa huduma za usafi kwenye maliwato za umma zilizopo katika vituo vikuu vya Mradi wa DART.

Akipokea gari hilo kutoka kwa mwakilishi wa Kampuni ya M/s Mohamed Builders Septemba 12, 2026, gari ambalo limetolewa kupitia utekelezaji wa kazi ya kuboresha miundombinu ya Awamu ya Kwanza kwa ufadhili wa Benki ya Dunia, Mtendaji Mkuu wa DART, Bw. Saidi Tunda, amesema hatua hiyo inaleta suluhisho la kudumu katika kukabiliana na changamoto za usafi.

“Hatua hii inaleta suluhisho la kudumu katika kukabiliana na changamoto za usafiri zilizokuwa zikitokea mara kwa mara kutokana na wingi wa abiria wanaotumia vituo hivyo kila siku,” alisema Bw. Tunda.

Aliongeza kuwa kupatikana kwa gari hilo kutapunguza utegemezi wa watoa huduma wa nje na kuhakikisha kuwa maliwato katika vituo vya Kimara, Ubungo, Gerezani, Kivukoni, Morocco, na Mbagala zinasafishwa na kuhudumiwa kwa wakati.

Aidha, Mtendaji Mkuu huyo alieleza kuwa gari hilo limekuja katika muda muafaka wakati Wakala ukifanya maandalizi ya kukabiliana na athari za mvua zinazotarajiwa kunyesha kuanzia mwisho wa mwezi Septemba 2026.

“Gari hili litakuwa msaada mkubwa sana. Lengo letu kuu ni kuhakikisha kuwa wananchi wanaendelea kupata huduma ya usafiri bila kukwama pindi barabara zinapofurika au zinapojaa maji kwenye vituo wakati wa mvua,” alifafanua Bw. Tunda.

“Litafanya kazi ya kunyonya na kuondoa maji hayo kwa haraka ili abiria waendelee kupata huduma kama kawaida.”

> “Hatua hii inaleta suluhisho la kudumu katika kukabiliana na changamoto za usafi zilizokuwa zikitokea mara kwa mara kutokana na wingi wa abiria wanaotumia vituo hivyo kila siku,”
>
> alisema Bw. Tunda.

Kuhusu mikakati ya dharura ya usafiri kipindi cha mvua, Bw. Tunda alibainisha kuwa daraja la Kigogo Sambusa na Mkwajuni katika Barabara ya Kawawa yatatumika kupitisha mabasi kuelekea katikati ya jiji endapo eneo la Jangwani litafurika maji na kushindwa kupitika, wakati ambapo ujenzi wa daraja la Jangwani ukiendelea.

“Wananchi wataendelea kupata huduma ya usafiri bila kukwama hata pindi mvua kubwa zitakaponyesha na kusababisha mafuriko Jangwani. Mabasi yetu yatatumia njia mbadala kupitia madaraja ya Kigogo Sambusa na Mkwajuni ili safari za kuelekea mjini zisiweze kusimama,” alisisitiza.

Gari hilo sehemu ya mpango wa dharura wa kukabiliana na mafuriko ya msimu wa mvua pamoja na matumizi ya njia mbadala wakati wa kufurika kwa eneo la Jangwani, ni mkakati wa DART katika kulinda uchumi wa jiji na kuhakikisha huduma za usafiri zinaendelea ikiwa ni nguzo muhimu katika kupunguza usumbufu kwa wakazi wa Dar es Salaam.

MAONESHO YA NaneNane

Usafiri wa Kisasa wa Mwendokasi wapewa sifa na wananchi Dodoma



Wanafunzi waliotembelea Banda la DART Dodoma

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) umeacha alama kubwa katika Maonesho ya 33 ya Kilimo maarufu Nanenane yaliyofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Dkt. Samuel Malecela jijini Dodoma, baada ya kuvutia mamia ya wananchi na wadau mbalimbali waliotembelea banda lake ili kujionea ubunifu wa mfumo wa usafiri wa umma nchini.

Maonesho hayo yalizinduliwa Agosti 1, 2026 na Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, yakiwa na kaulimbiu "tambua soko, ongeza tija kutekeleza dira ya maendeleo 2050," DART ilishiriki kupitia banda jumuishi la Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Akiongea muda mfupi baada ya kuhitimishwa maonesho hayo, aliyekuwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma DART, Bw. William Gatambi alisema zaidi ya wageni 900 walitembelea banda la DART kupata elimu ya miradi inayotekelezwa, kutoa ushauri na maoni kuhusu uboreshaji wa huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka.

"Katika kipindi chote cha maonesho, wageni zaidi ya 900 walitembelea banda letu kufahamu kuhusu miradi inayotekelezwa pamoja na kutoa maoni ya kuboresha huduma zetu Jijini Dar es Salaam na maeneo mengine." Alisema Bw.Gatambi.

Aidha Gatambi aliongeza kuwa moja ya vivutio vikubwa kwa wageni hao ilikuwa ni elimu kuhusu Programu tumizi ya Mwendokasi ikiwa ni njia mbadala ya kulipa nauli badala ya kutumia Kadi janja ya Mwendokasi.

"Ukataji wa tiketi kupia App ya Mwendokasi katika simu janja iliwavutia wengi," alisema Gatambi. "wamepongeza Wakala wa DART kwa namna unavyokwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia."

Hata hivyo baadhi ya wananchi na wanafunzi waliotembelea banda la DART walionesha shauku kubwa ya kutaka kufahamu ni lini huduma ya usafiri wa mabasi yaendayo haraka itatolewa kwenye maeneo mengine ya nchi hususani Dodoma.

"Kiu yangu kubwa ni kuona huduma ya mabasi ya Mwendokasi ikisambaa kwenye miji yenye msongamano wa vyombo vya moto kama jiji la Mwanza, au Dodoma ingawa Serikali imejitahidi kulipanga kwa kuwa na barabara za mzunguko." Alisema Simeo ambaye ni mkazi wa Dodoma.

Aidha kufikia ndoto hiyo, wananchi walifafanuliwa kuwa DART imekamilisha tafiti katika jiji la Tanga, Mbeya, Arusha, Mwanza, na Dodoma, kwa lengo la kutathmini uwezekano wa kuanzisha mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka ili kukabiliana na changamoto za msongamano na kuleta tija ya kiuchumi kwenye majiji hayo yanayokua kwa kasi.

Katika maonesho hayo ambayo yaliipa DART jukwaa la kukutana na wananchi, yalihitimishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Agosti 8, 2026 huku Mradi wa DART ukibaki kuwa nguzo muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi na kutimiza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

> "Katika kipindi chote cha maonesho, wageni zaidi ya 900 walitembelea banda letu kufahamu kuhusu miradi inayotekelezwa, pamoja na kutoa maoni ya kuboresha huduma zetu jijini Dar es Salaam na maeneo ya mengine."
>
> **Alisema Bw. Gatambi.**

Ruti mpya ya majaribio yaleta nafuu kubwa kwa Abiria wa katikati ya Jiji





Katika jitihada za kuendelea kuboresha huduma za usafiri wa umma na kupunguza kero ya msongamano wa vyombo vya usafiri binafsi mjini, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) umetambulisha njia mpya ya majaribio inayotokea Kivukoni hadi Gerezani kupitia ushoroba wa Awamu ya Pili ya Mradi wa DART.

Uanzishwaji wa ruti hiyo mpya umekuja kufuatia utafiti uliolenga kutatua changamoto za kiusafiri ulifanywa na DART kwa kushirikiana na Mtoa Huduma ya Mabasi ya Awamu ya Pili, Kampuni ya Mofat.

Awali, kabla ya kutambulishwa kwa njia hiyo mpya, abiria waliokuwa wakifanya safari kutoka Kivukoni kuelekea Gerezani walilazimika kutumia mabasi kuelekea Mbagala kupitia Mradi wa DART Awamu ya Pili na kushuka katika Kituo cha Bandari ili kubadilisha basi la kuelekea Gerezani.

Vilevile, kwa upande wa Mradi wa DART Awamu ya Kwanza, abiria waliotokea Kivukoni kuelekea Gerezani walilazimika kupanda mabasi ya kuelekea Kimara au Morocco hadi Kituo cha Fire ili wabadilishe basi kuelekea Gerezani.

Hata hivyo, uchunguzi uliofanywa kwa abiria ulibainisha kuwa wengi wao hawakupenda kuunganisha mabasi hayo, kwani mara nyingi yalikuwa yamejaa abiria wa vituo vya mwisho (kama Mbagala, Kimara, au Morocco), jambo lililowapa usumbufu mkubwa wakati wa kushuka katika vituo vya Fire au Bandari.

“Kuunganisha mabasi ni kitu nilikuwa nafanya, lakini kwa kuangalia ni nyakati zipi naweza kufanya hivyo,” alisema Glory Joseph, mkazi wa Kigamboni. “Nilikuwa sithubutu kufanya hivyo nyakati za jioni kwa sababu abiria ni wengi na hata kushuka ndani ya basi ni changamoto kubwa.”

Kutokana na changamoto hiyo, abiria walilazimika kutumia usafiri mbadala wa pikipiki za magurudumu mawili (bodaboda), magurudumu matatu (bajaji), au teksi za mtandaoni, kama anavyoeleza Hamis Kivembele, mfanyabiashara wa Kariakoo.

“Wewe mwenyewe unaona, ndugu mwandishi, bodaboda na bajaji walivyokuwa wengi hapa Feri. Wateja wao wakubwa ni sisi tunaoshuka kwenye pantoni. Kupanda Mwendokasi hadi Kariakoo ulikuwa usumbufu mkubwa kwangu hasa nyakati zenye abiria wengi,” alisema Hamisi.

Usafiri huo mbadala uliwagharimu fedha nyingi abiria hao, wakilipa nauli za shilingi 1,500 na zaidi, huku wakichelewa kwenye shughuli zao kutokana na msongamano kwenye barabara za kawaida na changamoto za kiusalama.

Hali hii ndiyo iliyochochea kuanzishwa kwa njia hiyo mpya mnamo Septemba 2, 2026, ili kutoa huduma nafuu kwa wakazi na wageni wenye shughuli zao katikati ya jiji.


Huduma hiyo mpya, ambayo mabasi yake husimama kupakia na kushusha abiria katika Vituo vya Posta ya Zamani, Water Front, na Kamata, mbali na kuokoa muda wa safari, inatajwa kufurahisha sana abiria, hasa wale wanaoelekea Kituo Kikuu cha Treni ya Umeme cha Magufuli.

“Nawashukuru sana uongozi wa Mwendokasi kwa kuliona hili. Sasa siwazi hata kipindi cha mvua, shilingi elfu moja yangu inanipeleka Kariakoo kwa raha mustarehe huku nikila kiyoyozi,” alisema Alphonse Zadock, mmoja wa wanufaika wa ruti hiyo.

Kuanzishwa kwa ruti hii ya majaribio ya Kivukoni hadi Gerezani ni ushahidi tosha wa jinsi Wakala wa DART unavyojikita katika kusikiliza kero za wananchi na kutafuta suluhisho za kiutendaji zinazogusa maisha ya kila siku.



Tunasikiliza



> **“Katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba 27, jumla ya simu 1,978 zilipokelewa kwenye call centre yetu na kupitia Mwendokasi portal jumbe 557 zilipokelewa na kufanyiwa kazi.”**
>
> **Alisema Bi. Hellen.**

DART inavyogeuza mrejesho kutoka kwa abiria kuwa chachu ya kuboresha huduma.

Katika mfumo wowote wa usafiri wa umma wa kisasa, mafanikio hayapimwi tu kwa wingi wa abiria wanaosafiri kila siku, bali yanapimwa kwa jinsi taasisi inavyosikiliza, kujali, na kuchukua hatua za haraka kutatua changamoto za wateja wake.

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) unaendelea kuweka viwango vya juu vya utumishi uliotukuka kupitia Kitengo chake cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma, ambacho kimekuwa daraja thabiti linalounganisha abiria na uongozi wa taasisi hiyo. Ripoti ya utendaji kazi ya kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba inatoa picha halisi ya taasisi inayofanya kazi kwa uwazi, inayowajibika, na inayothamini kila maoni, ushauri, na kero kutoka kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam.

Katika kipindi hicho cha miezi mitatu, DART ilithibitisha dhamira yake ya kusikiliza wananchi kwa kupokea na kushughulikia jumla ya hoja na maoni mbalimbali zaidi ya **2,746** kupitia njia zake rasmi za huduma kwa Wateja ikiwemo kituo cha miito ya simu (Call center) pamoja na mitandao ya kijamii.

Afisa Huduma kwa Wateja DART, Bi. Hellen Msovela anasema kupitia Kituo cha Miito ya Simu, abiria waliwasiliana na kituo kwa masuala mbalimbali ambapo simu 1,978 zilipokelewa kupitia namba 0800110147 huku jumbe fupi za maneno 557 zilipokelewa kupitia Program ya Mwendokasi (Mwendokasi App).

“Katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba 27, jumla ya simu 1,978 zilipokelewa kwenye call centre yetu na kupitia Mwendokasi portal jumbe 557 zilipokelewa na kufanyiwa kazi.” Alisema Bi. Hellen.

Aidha, Bi Hellen aliongeza kuwa Wakala ulipokea jumbe **166** kupitia kurasa zake za mitandao ya kijamii za Instagram, Facebook, na LinkedIn, huku jumbe nyingine **45** zilipokelewa kupitia baruapepe.

“Vilevile tulipokea jumbe 166 katika kurasa za mitandao ya kijamii ilhali jumbe **45** zilipokelewa kupitia baruapepe yetu ya mteja@dart.go.tz.” aliongeza Bi. Hellen “katika mawasiliano yalivyofanywa na abiria katika kipindi tajwa, maoni na ushauri **137** ulikusudia maboresho ya kiutendaji.”

Uwingi wa mawasiliano haya sio tu kwamba unaonyesha uaminifu mkubwa waliyonayo wananchi kwa DART, bali pia unaashiria utayari wa wakala kufungua milango ya mawasiliano ili abiria nao wajisikie kuwa sehemu ya maamuzi katika kuboresha huduma.

DART -Polisi wafanya Kampeni ya Usalama Barabarani kuzuia wavamizi



Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama barabarani wamefanya kampeni ya Usalama barabarani kwa lengo la kuelimisha umma juu ya matumizi sahihi ya Mundombinu ya DART.

Kampeni hiyo yenye lengo la kupunguza au kumaliza kabisa uvamizi wa barabara za Mabasi Yaendayo Haraka imekuja baada ya Wakala kushuhudia kukithiri kwa magari binafsi, pikipiki, bajaji, baiskeli na maguta katika barabara za hizo.

Akizungumzia kuhusu zoezi hilo Mkurugenzi wa Uendeshaji na Usimamizi wa Miundombinu wa DART Dkt. Philemon Mzee alisema, toka kuanzishwa kwa huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa sheria za usalama barabarani hasa matumizi yasiyofaa ya Barabara za Mwendokasi kwa vyombo visivyoruhusiwa.

Dkt. Mzee aliwakumbusha pia abiria wa Mabasi Yaendayo Haraka kuzingatia maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili ya kuingia na kutoka ndani ya vituo.

“Hairuhusiwi kwa abiria wa Mabasi Yaendayo Haraka almaarufu kama Mwendokasi kuruka na kutoka katika jukwaa la kupandia basi na kwamba atakayebainika kufanya hivyo atachukuliwa hatua kali za kisheria.” Alisema Dkt. Mzee.

Kwa upande wake Mkaguzi Msaidizi wa Polisi Bahati Lugano Anyomwile anayeshirikiana na DART katika zoezi hilo aliwataka wananchi na watumiaji wote wa barabara kuzingatia alama na sheria za usalama barabarani hususani matumizi sahihi ya vivuko vya waenda kwa miguu, alama za pundamilia, pamoja na madaraja ya juu na kujiepusha kabisa na kukatiza kiholela katika Barabara za Mwendokasi.

“Imekuwa ni tabia na mazoea kwa abiria na wananchi wa kawaida kuvuka katika maeneo ambayo siyo ya vivuko na wengine wakiwa wamevaa visikiliza sauti maarufu kama “earphones” hali ambayo imesababisha ajali nyingi. Nawasihi kutumia vivuko rasmi ama kwenye alama za pundamilia kwa ajili ya kuvuka.” Alisema Mkaguzi Msaidizi Bahati.

Pia aliwataka waendesha bodaboda au bajaji wanapovuka kutumia alama za pundamilia kushuka na kukokota bajaji au pikipiki wakati wa kuvuka ili kuepusha ajali zinazoweza kujitokeza wakati wakati wa kuvuka wakiwa wanaendesha.

Aidha, aliwataka wananchi wanaolala au kufanyia biashara ikiwemo shughuli za kuombaomba kwenye madaraja ya juu na kwenye vivuko kuacha mara moja tabia hiyo kwani madaraja hayo yamewekwa maalum kwa ajili ya kuvuka kwa waenda kwa miguu.

Zoezi hilo lilienda sambamba na utoaji wa elimu kwa umma juu ya matumizi sahihi ya miundombinu ya DART na kwa upande wa abiria wanaotumia Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka walipata elimu juu ya matumizi ya Program tumizi ya kukatia tiketi kidigitali (Mwendokasi App) ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza kwa wale ambao hawana Kadi za Mwendokasi. Elimu hiyo ilitolewa kwa abiria katika Awamu ya Kwanza ya Mradi kutokea Kimara, Gerezani na Kivukoni na Awamu ya pili ya mradi kutokea Gerezani hadi Mbagala Rangi Tatu.

> **“Hairuhusiwi kwa abiria wa Mabasi Yaendayo Haraka maarufu kama Mwendokasi kuruka na kutoka katika jukwaa la kupandia basi na kwamba atakayebainika kufanya hivyo atachukuliwa hatua kali za kisheria.”**
> **Alisema Dk. Mzee.**

FURSA ZA UWEKEZAJI KWENYE MRADI WA DART

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka DART unakaribisha wadau wa maendeleo makampuni ya ndani na ya kimataifa pamoja na wajasiriamali wadogo na wa kati kumchangamkia fursa zinazopatikana katika mradi. Karibu Ofisi za Wakala zilizopo Ubungo Maji Jijini Dar es Salaam ili kufahamu zaidi.







Wakala wa DART kuanza kuvuna matunda ya usafiri safi kupitia biashara ya kaboni

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) umeanza kuiendea fursa ya biashara ya kaboni kwa kuuza hewa ukaa ili kujiongezea mapato yasiotokana na nauli.

Itakumbukwa Agosti 7, 2026 wakati wa uzinduzi wa Mradi wa DART Awamu ya Pili kuelekea Mbagala, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Prof Riziki Shemdoe alimweleza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira watahakikisha wanatumia fursa ya matumizi ya Gesi kwenye Mabasi kama chanzo cha mapato.

"Mh.Rais kwakuwa Mabasi haya yanatumia nishati safi ya Gesi asilia mimi nitakaa na wenzangu na tutaangalia namna ya kupata fedha kwani tunapunguza sana hewa ya ukaa ambayo ingezalishwa kama Mabasi haya yasingetumia nishati hii ya gesi," alisema Waziri Shemdoe.

Sasa katika hali ya kawaida, mwananchi anaweza jiuliza ni namna gani DART inaweza kufanya biashara ya kaboni? Twende sawa.

Dunia kwa sasa inakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi na kupandisha joto la dunia. Hali hii inatokana na uzalishaji mkubwa wa hewa ukaa kwenye anga kutokana na shughuli za kibinadamu zinazopelekea kuchafua hewa na mazingira.

Uchomaji wa nishati ya mafuta kama vile petroli, dizeli na makaa ya mawe kwenye viwanda na magari, pamoja na ukataji wa miti hovyo kumechangia kwa kiasi kikubwa kwa ongezeko la hewa ukaa duniani. Aidha, mataifa mbalimbali ikiwemo Tanzania baada ya kuona ongezeko la hewa ukaa linalosababisha mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la joto, walikubaliana kwa pamoja kuweka mikakati ili kukabiliana na tatizo hili.

Mikakati mikuu iliyofikiwa na dunia ni pamoja na makubaliano yaliyomo kwenye mkataba wa Paris wa mwaka 2015, kuachana na nishati ya mkaa na mafuta, kulinda misitu na mimea, biashara ya kaboni pamoja na kufanya vikao vya kila mwaka ili kupima utekelezaji wa ahadi hizi. Makala hii itajikita katika ahadi ya nne ya Biashara ya kaboni iliyorasimishwa na kukubaliwa rasmi duniani kupitia Itifaki ya Kyoto Japan Desemba 11, 1997 wakati wa Mkutano wa 3 wa nchi wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi - COP3.



Kituo cha kujaza gesi kilichopo karakana ya Mbagala Rangi Tatu

Ingawa mkataba ulisainiwa mwaka 1997, mifumo ya kisheria na utekelezaji wake ilianza kufanya kazi rasmi baada ya mkataba huo kuanza kutumika mnamo Februari 2005.

Madhumuni ya Itifaki ya Kyoto yalikuwa ni kuruhusu nchi au kampuni zinazozalisha hewa ukaa nyingi kununua haki ya utoaji hewa kutoka kwa zile (nchi au kampuni) zinazohifadhi mazingira na kupunguza gesi hizo.

Hii ina maana kampuni ambayo katika shughuli zake za uzalishaji wa bidhaa umekuwa ukichafua sana mazingira kwa uzalishaji wa hewa yenye madhara, wanapaswa kulipa kiasi cha fedha au itakavyokubalika vinginevyo, nchi, taasisi au mtu binafsi ambao kwenye shughuli zao za kila siku wanatunza mazingira kwa kutozalisha hewa ukaa.
Kwa mfano mtu binafsi aliyepanda miti hekari nyingi ambazo zitathibitika kuvuta hewa chafu, anayo haki ya kuuza kiwango hicho cha hewa kilishosafishwa kwa kampuni iliyochafua na kujipatia kipato.

Soko au biashara hii ilipata nguvu mpya na kuwekewa sheria za kisasa zaidi kupitia Mkataba wa Paris wa mwaka 2015 uliofanyika nchini Ufaransa, ambapo kupitia Kifungu cha 6, dunia ilikubaliana upya kuhusu mfumo wa kimataifa wa biashara ya kaboni unaotumika hadi leo katika nchi mbalimbali duniani.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, ilianzisha Kituo cha Taifa cha Kufuatilia na Kuratibu masuala ya Kaboni ili kuiendea fursa hii. Kituo hiki kilizinduliwa tarehe 19 Mei 2016 katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine mkoani Morogoro na aliyekuwa Waziri wa

Inaendelea ukurasa 18

..... biashara ya kaboni

Inatoka ukurasa 17

.....kilizinduliwa tarehe 19 Mei 2016 katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine mkoani Morogoro na aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Mhe. Januari Makamba.

Tangu kuanzishwa kwake kituo kimeiwezesha Tanzania kunufaika na masoko ya kaboni na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kama alivyonukuliwa Mheshimiwa Mhandisi Hamadi Masauni akisema biashara ya kaboni ni fursa ya kiuchumi.

"Biashara ya Kaboni ni fursa ya kiuchumi kwa nchi yetu na wananchi wote," alisema Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais wakati wa kilele cha siku ya mazingira Juni 5, 2026 Jijini Dodoma.

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka umeiona fursa hii ya biashara ya kaboni na sasa umeanza mchakato wa kunufaika kwa kipato kitakachoongeza ukwasi katika mfuko wa mapato yasiyotokana na nauli.

Msingi kwa kunuifaika na biashara hiyo unajengwa kupitia Kifungu Na. 3 cha Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya 1997, inayoipa DART jukumu la kuanzisha na kusimamia utekelezaji na uendeshaji wa mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka Mkoa wa Dar es Salaam. Vilevile sheria hiyo inaipa nguvu Wakala wa DART kuweka mpangilio makini wa matumizi ya barabara kuu na mlishi kwa watumiaji wote ili kupunguza msongamano katika jiji.

Aidha, itakumbukwa kuwa tarehe 16 Mei 2016, huduma ya usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka ilianza kutolewa jijini katika Awamu ya Kwanza ya Mradi wa DART kutokea Kimara hadi Kivukoni, Gerezani na Morocco.

Hakika huduma hii ya usafiri ilikuwa ni mkombozi kwa wakazi na wageni wa jiji la Dar es alaam walioteseka kwa muda mrefu kutokana na msongamo wa magari barabarani.

Mateso hayo hayakuwa kwenye msongamano pekee, bali pia usafiri umma ulikuwa ni duni wenye mabasi madogo, yaliyochakaa na yenye kuchafua mazingira kwa uzalishaji wa hewa ukaa ambapo kiujumla haikumfanya mkazi wa jiji afurahie usafiri wa umma.

Jambo hilo linatolewa ushuhuda na Minael Elia mkazi wa Kimara aliyesema ilichukua saa mbili na dakika 30 kutokea Kimara hadi Kivukoni akitaja Ubungo kama eneo korofi kwa kipindi hicho.

"Kwakweli kila kitu kitabaki historia, eti leo hii tunatumia dakika 40 tu kufika Posta..mmh enzi zile tulitumia masaa mawili na nusu kufika," alisema Minael. "kuivuka tu Ubungo mataa ilikuwa kazi kwelikweli."

Changamoto hizo zilikoma baada ya huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka maarufu kama mwendokasi kuanza kutoa huduma, hali iliyopelekea uondoshwaji wa daladala na kuwafanya wasafiri wa binafsi kuacha kutumia vyombo vyao vya usafiri na kuhamia kwenye usafiri wa kisasa wa mabasi ya mwendokasi.

Usafiri huo unatajwa kuwa wa kisasa kwa kuwa ulibeba abiria wengi kwa wakati mmoja (150 mabasi marefu na 80 mafupi) na yakipita katika njia yake maalum huku abiria walio wengi ndani ya basi wakisafiri huku wamesimama kwa uhuru tofauti na kwenye daladala.

Usasa huo pia unatajwa kuwepo pia katika utunzaji wa mazingira. Mabasi ya mwendokasi yaliyotumika kipindi hicho yalikuwa na injini ambayo ni rafiki wa mazingira yakitumia mafuta masafi ya Euro III.

Sababu hizo zinaufanya Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka kuingia katika biashara ya kuuza kaboni kwani uwepo wake umeondoa uchafuzi wa mazingira kwa kiasi kikubwa.

Biashara hiyo pia inazidi kupewa msukumo na nguvu zaidi hata baada ya kuanza kwa huduma ya Mradi wa DART Awamu ya Pili kutokea katikati ya Jiji kuelekea Mbagala kama anavyobainisha Mhandisi Albina Griphin, Meneja Usimamizi wa Mazingira na Hifadhi ya Jamii DART.

Hifadhi ya Jamii DART.
"Katika juhudi za kuhakikisha tunaendelea kulinda na kutunza mazingira, tumekuwa na mpango mkakati wa kubadilisha nishati inayotumika katika mabasi kuelekea nishati safi kabisa ya gesi asilia na umeme."alisema Mhandisi Albina. "tulianza na mafuta na ingine za hali ya juu kama mpango wa muda mfupi, sasa mabasi yetu kuelekea Mbagala yanatumia gesi asilia kama mipango ya kati na matumizi ya umeme kama mpango wa muda mrefu kwenye mabasi yote ya DART."

Matumizi ya nishati ya gesi katika mabasi ni hatua ambayo DART mbali na kuondoa daladala zilizokuwa zikichafua mazingira na kuwafanya wasafiri binafsi kuhamia kwenye mabasi ya mwendokasi pia inatosha kwa taasisi hii kuingia katika biashara ya Kaboni.

Hilo pia linashuhudiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati akuhutubia bunge Novemba 14, 2025 kuwa Serikali inalinda mazingira kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.

"Tumeimarisha mazingira yetu kupitia miradi ya maendeleo ikiwemo biashara ya kaboni." Alisema Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania.

Ni wazi kuwa hadi kufikia 2035 inapokadiriwa kuwa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka utakuwa unatekelezwa katika awamu zote sita, Jiji la Dar es salaam litakuwa na uchafunzi finyu sana wa hewa ukaa huku Mradi wa DART ukitajwa kuwa kinara wa utunzaji wa mazingira.

Faida ya utunzaji huo wa mazingira utakwenda sambamba na kuongeza kipato kupitia biashara ya kaboni, kipato kitakachoiwezesha DART kuboresha huduma ya usafiri kwa wakazi wa Jiji huku fedha iyokuwa ielekezwe kwake na Serikali itakwenda kuhudumia wananchi maeneo mengine ya Tanzania.

"Kwakweli kila kitu kitabaki historia, eti leo hii tunatumia dakika 40 tu kufika Posta.. mmh enzi zile tulitumia masaa mawili na nusu kufika," alisema Minael. "kuivuka tu Ubungo mataa ilikuwa kazi kwelikweli."

Kutoka darasani hadi historia ya BRT: Safari ya William Gatambi ya mawasiliano na utumishi wa umma.



Makala maalum ya kuadhimisha kustaafu kwake kutoka Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) baada ya miaka 18 ya utumishi

Tarehe 28 Septemba 2026, William Venant Gatambi anafunga ukurasa muhimu wa utumishi wa umma baada ya kustaafu kutoka Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), ambako ametumikia kwa miaka 18. Anaondoka akiwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma, baada ya kutumia sehemu kubwa ya maisha ya Wakala akisaidia kujenga na kuimarisha namna taasisi inavyowasiliana na umma.

Safari ya Gatambi si simulizi ya mtaalamu wa mahusiano kwa umma aliyekaa ofisini kwa miaka mingi tu bali pia ni simulizi ya mtaalam wa mawasiliano ya umma aliyejiunga na DART wakati Wakala ukiwa katika hatua za awali za kuanzishwa hadi katika safari yenye changamoto, mahitaji makubwa na mafanikio ya kihistoria ya kuanzishwa kwa mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka jijini Dar es Salaam.

Wakala wa DART ilipoanzishwa mwaka 2008 kusimamia utekelezaji wa mfumo wa BRT katika awamu sita, Gatambi alikuwa miongoni mwa wataalamu waliosaidia kujenga kazi ya mawasiliano ya umma tangu mwanzo. Utumishi wake wa muda mrefu unamuweka miongoni mwa watumishi walioshuhudia, kushiriki na kuwasilisha kwa umma hatua nyingi zilizounda historia ya DART.

Kabla ya kujiunga na DART, Gatambi alikuwa tayari amejenga msingi mpana wa kitaaluma. Alianza uzoefu wake wa kazi akiwa mwalimu wa Hisabati na Kompyuta katika Shule ya Sekondari Loreto inayomilikiwa na Shirika la Masista Watawa wa Loreto, na Shule ya Sekondari ya Taqwa, Saqafa, vyote vikiwa jijini Mwanza. Uzoefu huo ulimjengea uwezo wa kufundisha, kueleza, kuwa na nidhamu na kufanya kazi na watu—ujuzi ambao baadaye ungekuwa muhimu katika mawasiliano na uhusiano kwa umma. Mwaka 2001, alihamia katika sekta ya maendeleo akiwa Afisa Mawasiliano katika Shirika lisilo la Kiserikali la Kuleana lililokuwa likishughulika na Watoto wa Mitaani, Mwanza. Nafasi hiyo ilikuwa hatua muhimu katika kuingia kwake katika taaluma ya mawasiliano na kumpa uzoefu wa vitendo katika utoaji wa taarifa, ujumbe wa taasisi na kuwafikia wadau wenye mahitaji na mitazamo tofauti.

Mwaka 2002, Gatambi alijiunga na Star TV, Mwanza, akiwa Mhariri Mkuu wa Habari. Kufanya kazi katika chumba cha habari chenye kasi kulimjengea zaidi uwezo wa kutambua habari, kuzingatia usahihi, kuheshimu muda, kufuata nidhamu ya uhariri na kuwasilisha taarifa kwa uwazi na uwajibikaji.

Mwaka 2004, alihamia Dar es Salaam na kujiunga na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), ambako alifanya kazi kwa zaidi ya miaka minne katika taaluma ya mawasiliano na uhusiano kwa umma. Uzoefu wake IFM uliimarisha zaidi uwezo wake wa mawasiliano ya kitaasisi kabla ya kukabiliana na jukumu kubwa zaidi la kuwasilisha kwa umma maendeleo ya programu muhimu ya usafiri wa umma.

Mwezi Mei 2008, Gatambi alijiunga na DART wakati Wakala ukiwa katika hatua za kujengwa. Kuanzia hapo, safari yake ya kitaaluma ikaunganishwa kwa karibu na maendeleo ya mfumo wa BRT wa Dar es Salaam. Hakuwa akiwasiliana kuhusu mradi uliokuwa tayari umekamilika; alikuwa akiwasiliana kuhusu programu ya umma iliyokuwa ikiendelea kubadilika katika miundombinu, uendeshaji, sera na huduma.

Moja ya sifa zilizojitokeza katika utendaji wake imekuwa msimamo wa kuwa mnyoofu na mwenye kulenga jambo katika mawasiliano ya kitaaluma. Katika masuala ya taasisi, taarifa kwa umma, maswali ya vyombo vya habari au changamoto za mawasiliano, amejitahidi kuweka ujumbe wazi, wa ukweli na unaohusiana na wajibu wa Wakala.
DART ilimpa fursa nyingi za kuutumia mtazamo huo. Programu ya BRT ilihusisha ujenzi, mabadiliko ya uendeshaji, matarajio ya wananchi, changamoto za huduma, awamu mpya na mifumo mipya. Kila hatua ilihitaji mawasiliano yaliyoweza kueleza kinachoendelea, sababu za hatua husika na maana yake kwa abiria na umma kwa ujumla.

Kwa sababu hiyo, Gatambi akawa sehemu ya sura ya mawasiliano ya DART mbele ya umma. Kupitia uongozi wake wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma, taarifa za Wakala ziliwafikia waandishi wa habari, abiria, wadau na wananchi kupitia njia mbalimbali kadri mfumo wa BRT ulivyokuwa ukipanuka.

Utumishi wake pia ulienda sambamba na mabadiliko ya DART kutoka taasisi iliyokuwa ikijikita zaidi katika utekelezaji wa awamu za mwanzo za BRT hadi taasisi inayosimamia mtandao unaokua na kujiandaa kwa awamu zinazofuata. Hivyo, alishuhudia safari kutoka ujenzi na kuanza kwa huduma za Awamu ya Kwanza hadi uendeshaji wa huduma za awamu nyingine na maendeleo ya awamu zilizofuata.

Mbali na mahusiano ya kawaida na vyombo vya habari, mawasiliano katika DART yalihitaji zaidi elimu na uhamasishaji wa umma. Masuala ya mwenendo wa abiria, usalama barabarani, matumizi ya njia maalumu za BRT, nauli, mifumo ya tiketi, mabadiliko ya huduma na matumizi ya majukwaa ya kidijitali yalihitaji mawasiliano endelevu. Jukumu la Gatambi lilimweka katikati ya jitihada hizo.

Safari yake ya kielimu imeenda sambamba na uzoefu wake wa kazi. Ana Shahada ya Sanaa katika Mawasiliano ya Umma kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino Tanzania (SAUT), Shahada ya Uzamili ya Biashara ya Kimataifa (MBA) kutoka IFM kwa ushirikiano na Institute of International Foreign Trade (IIFT), India, pamoja na masomo ya Falsafa na Teolojia kutoka Seminari Kuu ya Mtakatifu Anthony wa Padua, Ntungamo, na Seminari Kuu ya Mtakatifu Paulo Mtume, Kipalapala. Shauku yake ya kutafuta maarifa

Inaendelea ukurasa 13

..... Safari ya William Gatambi ya mawasiliano na utumishi wa umma.

Inatoka ukurasa 12

..... imeenda sambamba na uzoefu wake wa kazi. Ana Shahada ya Sanaa katika Mawasiliano ya Umma kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino Tanzania (SAUT), Shahada ya Uzamili ya Biashara ya Kimataifa (MBA) kutoka IFM kwa ushirikiano na Institute of International Foreign Trade (IIFT), India, pamoja na masomo ya Falsafa na Teolojia kutoka Seminari Kuu ya Mtakatifu Anthony wa Padua, Ntungamo, na Seminari Kuu ya Mtakatifu Paulo Mtume, Kipalapala.

Shauku yake ya kutafuta maarifa imeendelea katika maisha yake yote ya kazi. Wakati wa kustaafu, alikuwa akihitimisha masomo yake ya Shahada ya Uzamivu (PhD) katika Mawasiliano ya Umma SAUT, Kampasi ya Dar es Salaam. Juhudi hizi zinaonyesha kiu ya kuendelea kujifunza, kufanya utafiti na kutafuta maarifa kwa njia ya kitaaluma.

Watumishi wenzake pia wanamhusisha Gatambi na utamaduni mkubwa wa kusoma. Vitabu, majarida na magazeti vimekuwa sehemu muhimu ya maisha yake binafsi na kitaaluma, na maktaba yake binafsi inaelezwa kuwa kubwa na yenye vitabu vya aina mbalimbali. Kwake, kununua kitabu kumekuwa uwekezaji katika maarifa zaidi kuliko gharama.

Miaka yake DART pia imejengwa na mahusiano yake na watumishi wa ngazi mbalimbali. Watumishi wenzake wamemuelezea kama mtu anayefikika kwa urahisi, mcheshi na anayeweza kushirikiana na watumishi wa umri na majukumu tofauti. Sifa hizo zilisaidia kujenga mahusiano ya kikazi yaliyovuka mipaka ya vyeo na taratibu rasmi za ofisi.

Nje ya ofisi, Gatambi amejiwekea utambulisho mwingine—mkulima na mfugaji. Katika shamba lake la Njianne, Wilaya ya Mkuranga, anajishughulisha na kilimo cha mazao mbalimbali, yakiwemo nyanya na mazao mengine ya chakula na biashara, pamoja na ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku. Kilimo kimekuwa sehemu muhimu ya maisha yake na mipango yake baada ya ajira rasmi.



Aliyekuwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma DART Bw. William Gatambi akizungumza na waandishi wa habari wakati wa utekelezaji wa majukumu yake.

Kwa hiyo, kustaafu kwake si mwisho wa shughuli za uzalishaji. Ni mwanzo wa ukurasa mpya ambao uzoefu alioupata katika mawasiliano, utumishi wa umma, elimu na kilimo unaweza kutumika kwa namna nyingine.

Utayari wake wa kutoa ushauri wa kitaaluma pale utakapohitajika pia una maana kwamba uzoefu wake utaendelea kuwa rasilimali hata nje ya ofisi anayoiaga.

Kwa kutazama nyuma, kazi ya Gatambi inaonyesha safari kutoka darasani kwenda mawasiliano ya maendeleo, kutoka chumba cha habari kwenda mahusiano ya umma ya kitaasisi, na hatimaye kuwa kiongozi wa mawasiliano katika taasisi kubwa ya usafiri wa umma. Kila hatua ilichangia kujenga hatua iliyofuata na kumwandaa kwa miaka 18 ya kusaidia DART kuwasilisha kwa umma dhamira na safari yake.

Anapoondoka katika utumishi wa umma, urithi wake unaweza kuonekana si katika kampeni au bidhaa moja ya mawasiliano pekee, bali pia katika kumbukumbu ya taasisi aliyoisaidia kujenga na watu aliokuwa akifanya nao kazi. Miaka 18 katika DART imeunganisha jina lake na kipindi muhimu cha historia ya mfumo wa BRT jijini Dar es Salaam.

Kwa DART, na hususan Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma, kustaafu kwa Gatambi ni kuondoka kwa mfanyakazi wa muda mrefu, mshauri na shahidi wa safari ya taasisi. Safari yake inaonyesha namna uthabiti wa kitaaluma, kujifunza bila kuchoka, mawasiliano ya moja kwa moja na kujituma katika utumishi wa umma vinavyoweza kujenga taaluma. Anapoanza ukurasa wake mpya, Wakala na wenzake wanamtakia maisha mema ya kustaafu, mafanikio na kila la heri katika miaka ijayo.

UTUMISHI

DART JARIDA **Toleo la 6** Julai - Septemba **2026**

DART yapokea waajiriwa wapya ili kuongeza ufanisi kiutendaji

Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba mwaka huu, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) umepokea waajiriwa wapya sita kwa ajili ya kuendelea kuboresha utendaji kazi.


Waajiriwa hao wapya ambao wamejiunga na Wakala katika kipindi hicho ni Bw. Salum Mussa Mtonga ambaye ni Afisa Msaidizi wa Huduma kwa wateja, Bi. Lucy Didas Sigula ambaye ni Afisa Sheria Daraja la II, pamoja na Bw. Davis Ahimidiwe Lema ambaye ni Afisa Uhakiki wa Ubora Daraja la II.

Wengine katika waajiriwa hao wapya ni Bw. Frank Totnan Bavon ambaye ni Afisa Masoko Daraja la II, Bw. Joseph Simon Misana Mhandisi Ujenzi Daraja la II, pamoja na Bi. Uria Amos Chaula ambaye ni Mtakwimu Daraja la II.

DART kama Taasisi nyingine za serikali zilivyo imeendelea kuboresha huduma za kiutumishi kwa kuzingatia ikama yake na mahitaji ya kiutumishi ili kuendelea kutoa huduma bora ya usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam.

Aidha, Wakala umekuwa ukijaza nafasi mbalimbali za watumishi kwa kuzingatia taratibu na miongozo ya utumishi wa umma ikiwemo nafasi za waajiriwa wapya serikalini pamoja na nafasi za wanaohamia kutoka katika taasisi mbalimbali za Serikali.

Kwa kuzingatia muundo na ikama yake Wakala wa DART kwa sasa una jumla ya watumishi 135 ambao ni waajiriwa wa kudumu.



SALUM MUSSA MTONGA
Afisa Msaidizi wa Huduma kwa Wateja



LUCY DIDAS SIGULA
Afisa Sheria Daraja la II



DAVIS AHIMIDIWE LEMA
Afisa Uhakiki wa Ubora Daraja la II.



FRANK TOTNAN BAVON
Afisa Masoko Daraja la II,



JOSEPH SIMON MISANA
Mhandisi Ujenzi Daraja la II



URIA AMOS CHAULA
Mtakwimu Daraja la II.

Taswira na matukio ya utekelezaji wa Mradi wa DART

UZINDUZI WA BRT AWAMU YA PILI



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan akiskani kadi ya Mwendokasi kwenye geti janja Kituo cha Water Front alipotumia usafiri wa BRT kuelekea Mtoni Kwa Aziz Ali, tarehe 7 Agosti, 2026.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwapungia mkono wananchi alipotumia usafiri wa BRT kuelekea Mtoni Kwa Aziz Ali tarehe 7 Agosti 2026.

ABIRIA



Abiria wakiingia kwenye basi katika Kituo Kikuu cha Kivukoni

MAKABIDHIANO YA NYARAKA



Mtendaji Mkuu DART Bw. Said Tunda akipokea nyaraka za gari maalum la majitaka kutoka kwa mwakilishi wa kampuni M/s Mohamed Builders Septemba 12, 2026

Taswira na matukio ya utekelezaji wa Mradi wa DART

UKAGUZI BENKI YA DUNIA



Maafisa kutoka Benki ya Dunia, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) pamoja na maafisa wa DART wakiwa katika ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa Miundombinu ya BRT Awamu ya Nne katika eneo la Tegeta tarehe 21, Septemba, 2026.

MFUMO WA KUONGOZEA MAGARI (ITS)



Timu ya Wataalam kutoka Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) pamoja na Wataalam kutoka Kampuni ya DERM Group wakiwa kwenye ziara ya ukaguzi wa miundombinu ya BRT Awamu ya Kwanza ikiwa ni hatua za awali za maandalizi ya usimikaji wa Mfumo wa Kuongozea Mabasi yaani Intelligent Transportation System (ITS)

KIKAO BODI YA USHAURI



Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wizara kwa Wakala Bw. David Kafulila (aliyesimama) akitoa neno la shukrani kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI Profesa Riziki Shemdoe (wa kwanza kushoto) alipozindua Bodi hiyo Julai 31, 2026.

KAMPENI YA USALAMA BARABARANI



Mkaguzi wa Jeshi la Polisi akitoa elimu ya matumzi sahihi ya Miundombinu ya BRT katika eneo la Msimbazi Kariakoo.

Taswira na matukio ya utekelezaji wa Mradi wa DART

MATUMIZI SAHIHI YA MAGETI JANJA



Abiria wakipatiwa maelezo kutoka kwa wasimamizi wa vituo namna ya kutumia Kadi ya Mwendokasi na App ya Mwendokasi katika mageti janja katika Kituo Kikuu cha Mbagala.

MAONESHO SABASABA



Mwananchi akipata ufanunuzi namna ya kutumia App ya Mwendokasi katika maonesho ya Sabasaba

MAONESHO YA NANENANE



Baadhi ya wananchi wakipatiwa maelezo kutoka kwa watumishi wa DART katika maonesho ya Siku ya Wakulima Nanenane yaliyofanyika jijini Dodoma

WAAJIRIWA WAPYA



Mkurugenzi wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Utawala wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka - DART Dkt. Eliphas Mollel, akiteta jambo na waajiriwa wapya wa Wakala wakati wa kikao kilichofanyika Septemba 4, 2026, Ubungo jijini Dar es Salaam.

DART
DAR RAPID TRANSIT AGENCY

DART JARIDA Toleo la 6 Julai - Septemba 2026

BRT TANGAZO

PAKUA MWENDOKASI APP

Ili uweze kukata tiketi ya Mabasi Yaendayo Haraka

FUATA HATUA HIZI UNAPOKATA TIKETI

Chagua Kituo cha kupandia kisha bidhaa yaani Trunk au Feeder

Chagua idadi ya tiketi au chagua kama unataka kumnunulia mwingine

Skani tiketi yako yenye alama ya msimbokodi yaani QR CODE kwenye geti janja

